05

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## MEI, 2025

Funded by the European Union

**20 JUNI, 2025**

## TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA MEI, 2025

### UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukioyaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.

### LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera nawatoa maamuzi.

### MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 107 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Mei, 2025 ambapo waathirika walikuwa 107. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 88.8, wakifuatiwa na wanawake asilimia 9.3 na wanaume asilimia 1.9.


Miongoni mwa watoto waathirika (waathirika 95), wasichana walikuwa 86 (asilimia 90.5) na wavulana walikuwa tisa (9) (asilimia 9.5).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mei 2025**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 68, ambapo waathirika 62 walikuwa wasichana na sita (6) wanawake. Matukio ya kulawiti/kunajisi yalikuwa tisa (9) ambapo waathirika wote walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa 12 ambapo waathirika 10 walikuwa wasichana na wawili (2) wanawake. Matukio ya kutorosha yalikuwa 11 ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya shambulio la aibu /kukashifu yalikuwa manne (4) ambapo waathirika wawili (2) walikuwa wanawake na waathirika wawili (2) wasichana, matukio ya mauaji yalikuwa mawili ambapo waathirika wote ni waname na tukio la wizi watoto lilikuwa moja ambapo muathirika alikuwa msichana.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio Mei, 2025**




Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine, matukio 23 sawa na asilimia 21.5 ikifuatia wilaya ya Magharibi 'B' ambapo yameripotiwa matukio 22 (asilimia 20.6). Wilaya ya Chakechake na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio mawili (2) kwa kila wilaya sawa na asilimia 1.9.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mei, 2025**



Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 4.9 kufikia matukio 107 kwa mwezi Mei, 2025 ikilinganishwa na matukio 102 kwa mwezi wa Aprili, 2025. Matukio mengi yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Mei, 2025 isipokuwa matukio ya kubaka, shambulio la aibu au kukashifu na kutupa watoto yamepungua. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2025 (matukio 23 ) na Kati iliongoza kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Aprili, 2025 (matukio 16).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Aprili 2025 na Mei, 2025**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kujaribu Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei |
| Kaskazini 'A' | 8 | 8 | 6 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 4 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 16 | 16 | 11 | 12 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| Kusini | 5 | 5 | 3 | 5 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 12 | 18 | 11 | 12 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 15 | 23 | 10 | 13 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 2 | 5 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 13 | 22 | 10 | 14 | 0 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 |
| Wete | 6 | 4 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Micheweni | 4 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Chake Chake | 10 | 2 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mkoani | 9 | 2 | 3 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **102** | **107** | **71** | **68** | **1** | **9** | **6** | **9** | **0** | **0** | **5** | **12** | **5** | **11** |

**Inaendelea....Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Aprili 2025 na Mei, 2025**

| Wilaya | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Mauaji | | Kutupa Watoto | | Wizi wa Watoto | |
| | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **0** | **0** | **13** | **4** | **0** | **2** | **1** | **0** | **0** | **1** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 37.8 kufikia matukio 107 kwa mwezi Mei, 2025 kutoka matukio 172 kwa mwezi wa Mei, 2024. Matukio mengi yameripotiwa kupungua kwa mwezi Mei, 2025 isipokuwa tukio la kulawiti/kunajisi na shambulio la aibu/kukashifu. Wilaya ya Magharibi ‘A’ ina idadi kubwa ya matukio kwa Mei, 2025 (matukio 23 ) na wilaya ya Mjini ilikuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2024 (matukio 45).

**Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Mei 2024 na Mei, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kujaribu Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 8 | 4 | 5 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 4 | 8 | 3 | | 0 | 1 | 0 | | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 10 | 16 | 6 | 12 | | 0 | 2 | 0 | | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Kusini | 4 | 5 | 2 | 5 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 45 | 18 | 20 | 12 | | 0 | 4 | 3 | | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 37 | 23 | 14 | 13 | | 0 | 2 | 3 | | 0 | 2 | 5 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 34 | 22 | 15 | 14 | | 0 | 3 | 3 | | 0 | 2 | 3 | 0 | 2 |
| Wete | 8 | 4 | 4 | 1 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 |
| Micheweni | 4 | 3 | 2 | 1 | | 0 | 2 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Chake Chake | 10 | 2 | 3 | 1 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 |
| Mkoani | 7 | 2 | 1 | 1 | | 0 | 1 | 0 | | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **172** | **107** | **79** | **68** | | **0** | **15** | **9** | | **0** | **9** | **12** | **9** | **11** |

**Inaendelea....Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Mei 2024 na Mei, 2025**

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shambulio | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Mauaji | | Wizi wa Watoto | | Usumbufu wa Kingono | |
| | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 |
| Kaskazini 'A' | 0 | | 0 | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | | 0 | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kati | 0 | | 1 | 0 | | 2 | | 0 | | 0 |
| Kusini | 0 | | 1 | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Mjini | 15 | | 4 | 1 | | 0 | | 1 | | 0 |
| Magharibi 'A' | 13 | | 5 | 1 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Magharibi 'B' | 11 | | 3 | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Wete | 0 | | 1 | 1 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Micheweni | 0 | | 0 | 1 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Chake Chake | 0 | | 3 | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Mkoani | 0 | | 3 | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| **Jumla** | **39** | | **21** | **4** | | **2** | | **1** | | **0** |

Miongoni mwa watoto 95 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Waliobakwa walikuwa wasichana 62, waliolawitiwa/kunajisi walikuwa wavulana tisa (9), kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana 10, kutorosha walikuwa wasichana 11, shambulio la aibu/kukashifu wasichana wawili (2) na wizi watoto msichana mmoja.

**Jadweli 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Mei, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Wizi wa Watoto | |
| | | Wasichana | Wavuala | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 8 | 5 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 13 | 11 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 16 | 12 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 18 | 10 | 3 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 20 | 12 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 4 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **95** | **62** | **9** | **10** | **11** | **0** | **2** | **0** | **1** | **0** |

Miongoni mwa wanawake 10 ambao ni waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa sita (6), kuingilia kinyume na maumbile wawili (2) na Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wawili (2).

**Jadweli 1.5: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Mei, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Mauaji | Kutupa Watoto |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 5 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **10** | **6** | **0** | **2** | **0** | **2** | **0** | **0** |

Kwa mwezi wa Mei 2025, Jumla ya matukio mawili (2) tu yaliripotiwa kwa wanaume, ambapo wote waliripotiwa kwenye tukio la mauaji.

**Jadweli 1.6: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Mei, 2025**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Mauaji | Wizi wa Watoto |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **0** | **0** | **0** | **2** | **0** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 50) sawa na asilimia 57.5 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 24) sawa na asilimia 27.6. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 40) sawa na asilimia 64.5 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.7: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Mei, 2025**

| Umri | 0-5 | | 6-10 | | 11-14 | | 15-17 | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** |
| Kubaka | 1 | | 7 | | 14 | | 40 | | 62 | |
| Kujaribu Kubaka | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 1 | | 2 | | 5 | | 1 | | 9 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 1 | | 7 | | 1 | | 1 | | 10 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 8 | 0 | 11 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wizi wa watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **3** | **1** | **15** | **2** | **19** | **5** | **49** | **1** | **86** | **9** |

Idadi ya matukio ya watoto kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 11.8 kufikia matukio 95 kwa mwezi wa Mei 2025 ikilinganishwa na matukio 85 yaliyoripotiwa mwezi wa Aprili 2025. Matukio yaliyoripotiwa kuongezeka kwa mwezi Mei 2025 ni kulawiti/kunajisi, kuingilia kinyume na maumbile, kutorosha na wizi wa watoto.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Aprili, 2025 na Mei, 2025**

| Miaka | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Mauaji | | Kutupa Watoto | | Wizi wa Watoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 | 25-Apr | Mei - 25 |
| 0-5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 4 |
| 6-10 | 3 | 7 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 7 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 17 |
| 11-14 | 9 | 14 | 1 | 0 | 2 | 5 | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 24 |
| 15-17 | 51 | 40 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 1 | 2 | 8 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 59 | 50 |
| **Jumla** | **63** | **62** | **1** | **0** | **6** | **9** | **4** | **10** | **4** | **11** | **6** | **2** | **0** | **0** | **1** | **0** | **0** | **1** | **85** | **95** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 33.6 kufikia matukio 95 kwa mwezi wa Mei 2025 ikilinganishwa na matukio 143 yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Mei 2024. Matukio mengi yameripotiwa kupungua kwa mwezi Mei 2025 kutoka Mei 2024 isipokuwa tukio la kuingilia kinyume na maumbile na kutorosha.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Mei, 2024 na Mei, 2025**

| Miaka | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Mauaji | | Wizi wa watoto | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 | Mei 24 | Mei - 25 | Mei - 24 | Mei - 25 |
| 0-5 | 3 | 1 | | 0 | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | | 0 | | 1 | 0 | | 10 | 4 |
| 6-10 | 5 | 7 | | 0 | 7 | 2 | 2 | 7 | 0 | 0 | 8 | 1 | | 0 | | 0 | 5 | | 27 | 17 |
| 11-14 | 18 | 14 | | 0 | 2 | 5 | 3 | 1 | 2 | 3 | 1 | 1 | | 0 | | 0 | 6 | | 32 | 24 |
| 15-17 | 44 | 40 | | 0 | 3 | 1 | 2 | 1 | 7 | 8 | 5 | 0 | | 0 | | 0 | 13 | | 74 | 50 |
| **Jumla** | **70** | **62** | | **0** | **15** | **9** | **8** | **10** | **9** | **11** | **17** | **2** | | **0** | | **1** | **24** | | **143** | **95** |

Matukio mengi (matukio 46) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 43.0 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea majumba mabovu (matukio 22) sawa na asilimia 20.6 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwezi Mei 2025.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Mei, 2025**





Matukio 93 kati ya matukio 107 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 86.9 ya matukio yote yaliyoripotiwa aidha matukio 11 yamepewa hati ya mashtaka (asilimia 10.3) na matukio matatu (3) yapo mahakamani (asilimia 2.8).

**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Mei, 2025**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | | | Hatua Zilizofikia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watoto | | Watu Wazima | | | | | | | | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi | Hati ya Mashtaka |
| Kubaka | 68 | 62 | | 6 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 59 | 7 |
| Kulawiti/Kunajisi | 9 | | 9 | | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 2 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 12 | 10 | | 2 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 2 |
| Kutorosha | 11 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Mauaji | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Wizi wa Watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **86** | **9** | **10** | **2** | **3** | **0** | **0** | **0** | **0** | **93** | **11** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwezi wa Mei 2025 walikuwa 107 kati yao 41 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 38.3, watu wasiojulikana walikuwa 31 sawa na asilimia 29.0 , jirani walikuwa 25 sawa na asilimia 23.4 na watu wengine walikuwa 10 sawa na asilimia 9.3

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Mei, 2025**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR MEI, 2025

Jumla ya Majalada 45 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Mei, 2025 ambayo yalihusisha makosa 47.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 30) sawa na asilimia 63.8 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Mei,2025**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 3 | 3 |
| Kusini Unguja | 7 | 7 |
| Mjini Magharibi | 28 | 30 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 4 |
| Kusini Pemba | 1 | 1 |
| Makao Makuu | 2 | 2 |
| **Jumla** | **45** | **47** |

Jumla ya Majalada 45 ya Udhalilishaji yameripotiwa kupokelewa kwa mwezi wa Mei, 2025, kati ya hayo,majalada 23 yameruhusiwa kwenda mahakamani, majalada tisa (9) hayajatolewa uamuzi, majalada nane (8) yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi na majalada matano (5) yamependekezwa kufungwa.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Mei 2025**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Kusini Unguja | 7 | 4 | 0 | 1 | 2 |
| Mjini Magharibi | 28 | 14 | 5 | 6 | 3 |
| Kaskazini Pemba | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini Pemba | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| **Jumla** | **45** | **23** | **5** | **8** | **9** |

Miongoni mwa makosa 47 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 34) sawa na asilimia 72.3 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Mei 2025**

| Mkoa | Jumla ya Makosa Kwenye Majalada Yaliopokelewa | Aina ya Ukatili Na Udhalilishaji Wa Kijinsia | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kutoros ha | Kujaribu Kubaka | Kubaka | Kubaka kwa Kundi | Kujaribu Kulawiti | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kulawiti | Usumbufu wa Kingono |
| Kaskazini-Unguja | 3 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini-Unguja | 7 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mjini Unguja | 30 | 1 | 0 | 22 | 0 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini-Pemba | 4 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini-Pemba | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Makao-Makuu | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **47** | **1** | **1** | **34** | **0** | **2** | **4** | **2** | **2** | **1** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA MEI 2025

Jumla ya mashauri 25 ambayo yanahusisha makosa 31 yamefunguliwa katika mahkama za udhalilishaji kwa mwezi wa Mei, 2025 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa yanayohusisha mashauri 16 (makosa 20) sawa na asilimia 64.0 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Mei, 2025**




Kati ya mashauri 25 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri yote bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Kesi za Ukatili na Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahkama na hatua zilizochukuliwa Mei 2025**

| Aina ya makosa | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa Hatiani | | | | | Zisizo na Hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia | Zilizoachiwa huru | Zilizondoshwa/Zilozfutwa |
| kubaka | 9 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka kwa kundi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kubaka na kutorosha | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jaribio la kubaka | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kutorosha | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **25** | **25** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

Jumla ya makosa 31 yaliyopokelewa katika Mahkama za udhalilishaji wa kijinsia , makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 15) sawa na asilimia 48.4 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Makosa ya Ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa Mei, 2025**

| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kubaka | 0 | 2 | 11 | 2 | 0 | 15 |
| Jaribio la kubaka | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 7 |
| Kulawiti | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| kutorosha | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1** | **4** | **20** | **4** | **2** | **31** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 107 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Mei, 2025 ambapo waathirika walikuwa 107. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 23) sawa na asilimia 21.5 Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 37.8 kufikia matukio 107 kwa mwezi Mei, 2025 kutoka matukio 172 kwa mwezi wa Mei, 2024

Matukio 93 kati ya matukio 107 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 86.9 ya matukio yote yaliyoripotiwa aidha matukio 11 yamepatiwa hati ya mashtaka (asilimia 10.3) na matukio matatu yapo mahakamani (asilimia 2.8).

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Mei, 2025**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Sehemu za kazi | | Skuli | | Madrasa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wanawake/ Wasichana** | **Wanaume /Wavulana** | **Wanawake /Wasichana** | **Wanaume /Wavulana** | **Wanawake /Wasichana** | **Wanaume /Wavulana** | **Wanawake /Wasichana** | **Wanaume /Wavulana** | **Wanawake /Wasichana** | **Wanaume /Wavulana** | **Wanawake /Wasichana** | **Wanaume /Wavulana** |
| Kubaka | 2 | | 29 | | 6 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 5 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 1 | | 6 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wizi wa watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **4** | **0** | **41** | **5** | **9** | **0** | **1** | **0** | **0** | **0** | **1** | **0** |

**Inaendelea.....Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Mei, 2025**

| **Sehemu Zilotokezea** | **Majumba mabovu** | | **Vichakani** | | **Vyombo vya usafiri(Gari)** | | **Fukwe za bahari** | | **Sehemu nyengine** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wanawake/Wasichana** | **Wanaume/Wavulana** | **Wanawake/Wasichana** | **Wanaume/Wavulana** | **Wanawake/Wasichana** | **Wanaume/Wavulana** | **Wanawake/Wasichana** | **Wanaume/Wavulana** | **Wanawake/Wasichana** | **Wanaume/Wavulana** |
| Kubaka | 16 | | 12 | | 0 | | 0 | | 3 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 3 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 2 | | 1 | | 0 | | 0 | | 2 | |
| Kutorosha | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wizi wa watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **19** | **3** | **15** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **6** | **3** |

Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mei, 2025

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Mauaji | | Wizi wa Watoto | |
| | | Wasichana/Wanawake | Wavulana/Wanaume | Wasichana/Wanawake | Wasichana/Wanawake | Wavulana | Wasichana/Wanawake | Wavulana | Wasichana/Wanawake | Wavulana | Wasichana/Wanawake | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 8 | 5 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 16 | 12 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 18 | 12 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 23 | 13 | 3 | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 22 | 14 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 4 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **68** | **9** | **12** | **11** | **0** | **4** | **0** | **2** | **0** | **1** | **0** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Aprili, 2025 na Mei, 2025**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Apr-25 | Mei-2025 | Apr-25 | Mei-2025 | Apr-25 | Mei-2025 | Apr-25 | Mei-2025 | Apr-25 | Mei-2025 |
| Kubaka | 71 | 68 | 8 | 6 | 63 | 62 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 6 | 9 | | | | | 6 | 9 | 0 | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | 0 | 0 | | | | | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 5 | 12 | 0 | 2 | 4 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 5 | 11 | 1 | 0 | 4 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 13 | 4 | 7 | 2 | 6 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kutupa Watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wizi wa watotot | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **102** | **107** | **16** | **10** | **78** | **86** | **7** | **9** | **1** | **2** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mei, 2024 na Mei, 2025**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 | Mei-2024 | Mei-2025 |
| Kubaka | 79 | 68 | 9 | 6 | 70 | 62 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 15 | 9 | | | | | 15 | 9 | 0 | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | 0 | 0 | | | | | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 9 | 12 | 1 | 2 | 8 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 9 | 11 | 0 | 0 | 9 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 21 | 4 | 4 | 2 | 13 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 39 | 0 | 7 | 0 | 11 | 0 | 13 | 0 | 8 | 0 |
| Mauaji | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wizi wa watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **172** | **107** | **21** | **10** | **111** | **86** | **32** | **9** | **8** | **2** |

**Jadweli 5.0 : Idadi ya Waathirika Wanawake na Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Mei 2025**

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jinsi | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume |
| Kubaka | 6 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 6 | |
| Kujaribu Kubaka | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 2 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mauaji | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wizi wa watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 8 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 10 | 2 |

**Jadweli 6.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea; Mei, 2025**

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 usiku | | 3:01 - 09:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jinsi | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana | Wanawake/Wasichana | Wanaume/Wavulana |
| Kubaka | 2 | | 5 | | 12 | | 14 | | 25 | | 10 | | 0 | | 0 | | 68 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 2 | | 6 | | 1 | | 0 | | 0 | | 9 |
| Kuingilia Kinyume | 0 | | 2 | | 1 | | 2 | | 4 | | 3 | | 0 | | 0 | | 12 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 11 | 0 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Wizi wa Watoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**